MUUNGANO wa KUTETEA HAKI za WATOTO

Kampeni Kuwalinda Watoto

FACTSHEET

Kwa nini haki za mtoto ni za msingi sana kwa maendeleo?

Nusu ya idadi ya watu Tanzania wako chini ya umri wa miaka 18. Maisha ya baadaye yanategemea ni jinsi gani leo tunavyowalea hawa vijana.

Asilimia hamsini ya idadi ya watu Tanzania ni watoto, je wanajaliwa vipi katika marekekebisho ya Sheria, Maendeleo ya Sera, bajeti ya kitaifa na zangazi za chini? Kampeni ya 50% inauliza: Tunawezaje kuendelea kama taifa wakati 50% ya idadi ya watu inatengwa na kubaguliwa?

Tunawataka watanzania kuongeza bidii katika kulinda na kutetea haki za watoto ili malengo ya kufuta umaskini yaweze kufikiwa. Kipeperushi hiki ni cha kwanza katika mfululizo wa vipeperushi vilivyoandaliwa na Muungano huu wakutetea Haki za Watoto ambavyo vianaelezea hali halisi ya watoto wa Tanzania.Tunaamini kwamba kwa kuuelimisha umma juu ya haki za watoto na umuhimu wake, tunaweza kuchochea utashi wa kisiasa juu ya kuwalinda watoto.

Katika kipeperushi chetu hiki cha kwanza, tunaelezea ni kwa nini kulinda haki za watoto ni muhimu kwa maendeleo ya taifa hivyo tunawaalika nyote kuingia kuchukua hatua katika kuwalinda watoto maishani mwenu.

Sote tulikuwa watoto. Sote tunawafahamu watoto. Sote tuna jukumu la kuboresha matakwa yao.



www.50campaign.org

Kampeni ya 50% Kuwalinda Watoto ni jitihada ya pekee ya kuchochea utambuzi wa kitaifa kwamba Tanzania ya kesho inategemea na jinsi tunavyowalea na tunavyowatendea watoto wetu leo, na kwa kwa sababu hiyo, kuna uhitaji wa haraka kufanya marekebisho ya kisheria, kuleta haki kwa vijana na watoto. Kwa habari zaidi juu ya kampeni hii na jinsi ya kujiunga tembelea tovuti yetu:

info@50campaign.org / www.50campaign.org

Muungano wa Kutetea Haki za Watoto (CCR) husaidia na kuratibu kampeni ya 50%. CCR imeundwa na watu binafsi pamoja na mashirika yaliyokubali wajibu wa kuwalinda watoto na vijana wa Tanzania. Uanachama unaruhusiwa tu kwa watu wenye fikra na maoni sahihi. Pata habari zaidi:

info@ccr-tz.org / www.ccr-tz.org

Huwa tunasikia juu ya HAKI ZA BINADAMU na HAKI ZA WATOTO, lakini ni zipi?

Haki si kitu cha makubaliano hivyo haki ni yakila mtu. Mwaka 1991 Tanzania iliungana na nchi nyingine duniani, sheria ya pili kuridhia Tamko la Umoja wa Mataifa juu ya Haki za Mtoto (UNCRC). Serikali ikafanya hivyo pia mwaka 2003 iliporidhia na kutia sahihi Hati ya Mkataba wa Afrika wa haki na Ustawi wa Mtoto. Hii inamaanisha yakwamba Serikali ya Tanzania ilikubali wajibu wa utaratibu wa mfumo mpya kabisa wa kimataifa ambao unawatambua watoto na vijana kuwa wenye haki. Serikali ya Tanzania ilikubali kuzilinda na kuzitetea haki hizo ili kuhakikisha kuwa maslahi bora ya watoto yanazingatiwa katika maamuzi yote ambayo yanawagusa. Kusudi ni kuwapa nafasi watoto wa Tanzania haki ya kuwa na afya, furaha na wenye kutoa mchango ndani ya jamii. Kwa sababu UNCRC ni sheria ya Kimataifa, Serikali ya Tanzania ilikubali kupitia tena ili kurekebisha na kuboresha sheria zake ili kulinda haki za watoto ndani ya nchi. Hili bado halijafanyika. 50% inatoa wito wa kupitiwa upya na kuboreshwa kwa Sheria ya Watoto na ikilazimu kutangua sheria zilizopitwa na wakati ambazo hazilindi haki za watoto.

Watoto wote wana mahitaji ambayo lazima yatimizwe ili waweze kukua na kuendelea. Kwa mfano, watoto wanahitaji familia yenye maisha salama, kulindwa na manyanyaso, uonevu na ubaguzi ili waishi na kusitawi (kufanikiwa). Mahitaji ya watoto na ustawi wao pamoja kuendelea kwao hakuwezi kutimizwa pasipo msaada wa watu wazima. Hii inawapa majukumu watu wazima watengeneze mazingira yanayofaa kuleta ustawi huo. Kukubali kwamba watu wazima wana wajibu au majukumu ya kutimiza mahitaji ya watoto pia ni kukubali kwamba watoto wana haki ya kutimiziwa mahitaji yao- kwamba wana haki. Shirika la UNCRC linaamini juu ya haki ambazo watoto wanastahili na linabainisha wajibu ambao watu wazima walio nao katika kuzilinda haki hizo.Wakati ambapo Serikali inaridhia haki hizo, mikataba kama ya UNCRC inatambulika kimsingi kuwa na wajibu wa kutunga sheria, sera na mipango ya utekelezaji wa kuwalinda watoto.Wazazi, familia na wanajamii wana wajibu wa kutetea haki za watoto. (Lansdowne, Erickson et al. 2009). Hii inamaanisha kwamba sote tuna jukumu la kulinda haki za watoto.

TATIZO NI NINI?

Kushindwa kuiingiza sheria ya watoto katika sheria za ndani kunawafanya watoto wabakie kuwa hatarini kwa sababu hakuna anaye weza kuwajibishwa kwa kushindwa kuwalinda. Wenye dhamana ya utekelezaji kama wafanyakazi wa ustawi jamii, walimu na wafanyakazi wa maendeleo ya jamii wanashindwa kutekeleza wajibu wao wa kuwalinda watoto kwa sababu ya kukosa nguvu na nyenzo/rasilimali. Mgawo wa rasilimali unakwama kwa sababu hakuna sheria ambayo kwa sasa inaendeleza na kutetea haki za watoto kwa hiyo mgawo wa rasilimali kwa ajili ya kupigania haki za watoto umewekwa kando/haupo.

Njia ya kuendeleza taifa iko katika kulinda na kutambua nguvu na uweza wa watoto, lakini hakuna utambuzi wa utashi wa kisiasa juu ta umuhimu wa swala hilo. Hii inaweza kuonekana katika kukosekana kwa huduma za kijamii na ulinzi kwa watoto.Swala hili linaonekana katika ngazi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto-wakati inawakilisha 75% ya idadi ya Wa-Tanzania wote, wizara hii ina bajeti ndogo zaidi na wala haikutoa changamoto kubwa au ushawishi mkubwa kwa Wizara ya Fedha. Mwisho, kukosekana kwa utashi huu wa kisiasa unaweza kuonekana katika mjadala wa Sheria ya Watoto ambao umekuwa ukiendelea toka mwaka 1994. Hii inaashiria kuwa watoto hawana umuhimu katika mitazamo ya watunga sheria na wahisani wetu. Tunawezaje kudai kwamba tunapambana kufikia malengo ya 2025 ya kuufuta umaskini wakati kazazi kijacho kimetengwa/tupwa kando kiasi hiki? Tunaujengaje uongozi wa kesho ikiwa hatuwekezi katika watoto leo?

TUNATAKA NINI?

Tunaishi katika demokrasia na hiyo inamaanisha kwamba kila mtu ana jukumu la kuuwajibisha uongozi kutetea haja ya kuwepo badiliko. Tunawahitaji watu wa kuiunga mkono Kampeni ya 50% na Watoto wa Tanzania wa waendelee kupigania kuleta mabadiliko. Kimsingi tunahitaji marekebisho ya kisheria ambayo yataingiza Sheria ya Watoto katika sheria za nchi.

Marekebisho ya sheria yanahitaji kupata maoni ya wadau wote, pamoja na watoto. Sheria hiyo iwe ya wazi na tunahitaji ahadi toka serikalini itoe muda maalum wa kumaliza mchakato wa kupata mashauri na kutoa Sheria ya "Haki za Watoto." (UN Committee on Rights of the Child 2006).

WITO KWA wataalam wote wa njia za mawasiliano! Kuwa MNAWEZA kupasha habari juu ya haja ya kuwa na utungaji sheria bora ambao unalinda watoto na kutimiza haja ya mgawanyo wa rasilimali kwa ajili ya huduma za watoto.

CALLING ALL donors and partners! YOU CAN use your influence to catalyse discussion in Government about a quality Children's Act.

WITO KWA watunga sheria wote! YOU CAN ask the Ministry of Justice and Minister for Community Development Gender and Children to table the Children's Act in Parliament.

WITO KWA wafanyabiashara wote! YOU CAN sponsor and raise awareness about 50% by using our logo and information on your corporate material.

Kama sehemu ya mchakato wa marekebisho ya sheria hii tunataka kanuni za kuondokana na ubaguzi ziwekwe bayana. " Ubaguzi wa makundi fulani ya watoto bado upo kwenye sheria na katika mipango ya kiutekelezaji pia, hususan kwa watoto wa kike wanaopata mimba, watoto wenye ulemavu, watoto wanaokimbia kutafuta hifadhi ya amani, watoto walioambukizwa na / au kuathirika na VVU/UKIMWI, na watoto wa mitaani. (UN Committee on Rights of the Child 2006).

Kushughulikia na kupinga ubaguzi huu kutaleta maana kwa kubatilisha au kurekebisha baadhi ya sheria za sasa ambazo kwa wazi kabisa zinabagua makundi fulani ya watoto. Kwa mfano Sheria ya Ndoa katika hali yake ya sasa inawabagua wasichana kwa kuwaruhusu waolewe wakiwa na umri wa miaka 15. Kwan in wasichana warusihusiwe kuolewa wakiwa bado watoto? Kwa nini umri ni tofauti kwa wavulana ambao wanaweza kuoa wafikiapo miaka 18?

Watoto wanaokumbana na sheria hii wako hatarini Tanzania. Sheria ya Watoto lazima ishughulikie ubaguzi na unyanyapaa wanaokumabana nao. Kwa kuanzia, sheria inahitaji "kuweka bayana umri wa kuwajibishwa kama mhalifu kuwa miaka 12 au zaidi ambao unakubalika katika viwango vya kimataifa. Itahitaji kuhakikisha kwamba watoto walio kati ya miaka 16 na 18 hawachukuliwi kuwa watu wazima na huvyo wapewe haki sawa na watoto wadogo chini ya mfumo wa haki wa watoto. " (UN Committee on Rights of the Child 2006)

Pia tunataka Sheria ya Watoto ambayo inawalinda watoto kinyume na vitendo vya kikatili na kuwavunjia heshima. Hii itamaanisha kufuta adhabu ya viboko katika mfumo wa adhabu, shuleni na katika taasisi mbadala za malezi. (UN Committee on Rights of the Child 2006). Sheria hiyo pia itahitaji kuweka utaratibu wa kushughulika na watoto ambao wamedhulumiwa/kuonewa kwa kuwekeza katika simu ya Msaada kitaifa kwa mtoto, dawati la kuwalinda watoto katika vituo vya polisi, vitengo mahospitalini ambapo watoto wanaweza kupatiwa ushauri nasaha na kuwa na benchi la watoto katika mfumo wa mahakama. Itahitaji fedha nyingi na jukumu kubwa toka Serikalini na wahisani, ambayo itachukua muda mrefu.

Unaweza Kufanya Nini?

Geuza karatasi; pata habari jinsi UNAVYOWEZA KULETA BADILIKO leo >>

Kanuni za Msingi za Haki ya Mtoto:

Haki ya Kuishi (Ibara ya 2) - Wakati ambapo mama na mtoto wanapaswa wawe wakipata mwendelezo wa huduma kabla ya kuzaliwa/kujifungua kwa njia ya chanjo, kwa vitendo ni 43% ya wamama hupata kuhudumiwa na mkunga mwenye ujuzi na 47% hupata huduma baada ya kuzaliwa.Kinachomaanishwa hapa ni kwamba siku ambapo hatari ya kifo iko juu sana, mama na mtoto wako mbali zaidi na huduma za kiafya. (Tanzania 2004-2005; Save the Children 2007).

Haki ya Kusikilizwa (Ibara ya 3) - Watoto wote wana haki ya kushiriki katika maamuzi yanayowagusa, kulingana na uwezo wao wa kukua.Kuna dhana miongoni mwa watu wazima kwamba watoto wachungwe na kusikilizwa. Katika mkutano hivi karibuni huko Pemba wakati wa kushirkishana matokeo ya utafiti kutokana na ushauri unaohusiana na watoto, afisa wa Serikali za Mitaa alikosa raha kutoa maoni yake kwa watoto, na asikubali maoni au maswali toka kwa watoto. (Save the Children 2007).Kama mtu mzima, je una maoni kuhusu maisha yako? Je ni vibaya kwa mtoto kuwa na juu ya maoni ya maisha yake? (Save the Children 2009).

Kutokubaguliwa (Ibara ya 6) - Mtoto anayeishi Tanzania ana haki sawa na mtoto anayeishi Uingeleza. Mtoto mwenye ulemavu ana haki sawa na mtoto asiye na ulemavu. Nchini Tanzania kwa nini hatujishughulishi zaidi kwa ajili ya watoto wetu?

Maslahi Bora ya Mtoto (Ibara ya 12) - Hivi karibuni Mkuu wa Wiliya fulani alikaripiwa kwa kutumia adhabu ya viboko kwa walimu. Na wakati watoto hupigwa mara kwa mara shuleni, nyumbani na sehemu hata sehemu waabudipo. Je, kweli ni kwa maslahi bora ya mtoto kupigwa na kudhalilishwa wakati haikubaliki kufanya hivyo kwa watu wazima?

Unaweza kufanya nini?

Sote tulikuwa watoto. Sote tunawafahamu watoto. Wote tuna jukumu la kuendeleza maslahi yao bora. Na hii inamaanisha kuchukua hatua ili kuleta badiliko-katika ngazi ya umma na kwa mtu binafsi.

Kama raia wa Tanzania UNAWEZA kuunga mkono 50% kwa kushawishi ili kuwepo na Sheria ya Watoto inayolinda Haki za Watoto. Mshirikishe Mbunge wako.Andika gazetini. Tia sahihi Ombi la 50%.

Kama Mtu Mzima, UNAWEZA kutambua uwezo na sauti za watoto. Skiliza kwa makini wasemayo kuhusu mambo wayapitiayo shuleni, nyumbani na katika jumuiya yako.

Kama Watu wazima WAJIBU WETU NI kulinda na kukiongoza kizazi kijacho. Hii inalazimu tuheshimu uwezo unaokua wa watoto, tuwaache waone/wapime ujuzi wao na kuwa na haki ya kusema/kutoa maoni, kuwaleimisha kwa kuwashirikisha na si kuwanyamizisha.

Wasikilize watoto wako.Waongoze/Wape ushauri. Linda Haki zao nyumbani.

REFERENCES:

United Nations Committee on the Rights of the Child (2006) CONSIDERATION OF REPORTS SUBMITTED BY STATES PARTIES UNDER ARTICLE 44 OF THE CONVENTION Concluding observations: United Republic of Tanzania.

Save the Children, (2007). Child Rights Situation Analysis - Health Tanzania, Save the Children.

Save the Children, (2007). Zonal feedback session for baseline survey in Pemba; Gombani Stadium, Save the Children in Tanzania - Change for Children Programme.

Save the Children, (2009). Change for Children in Zanzibar.

Lansdowne, G., M. Erickson, et al. (2009). A training course on child rights for Tanzanian professionals working with young children (DRAFT), CRED PRO, MS TCDC & Bernard Van Leer Foundation.

Tanzania, U. R. o. (2004-2005). Tanzania Demographic and Health Survey. Dar es Salaam, National Bureau of Statistics.

CCR Muungano wa Kutetea Haki za Watoto

Muungano wa Kutetea Haki za Watoto
P.O. Box 11372
Mt. Meru Post Office
Arusha, Tanzania

info@ccr-tz.org
www.ccr-tz.org

MUUNGANO WA KUTETEA HAKI ZA WATOTO INATAAMALI kwamba Tanzania ilinde haki za watoto wake wote; kwamba haki za watoto wote wa Ki-Tanzania zipashe habari sera na mipango ya utekelezaji; kwamba "maslahi bora" ya watoto wa Ki-Tanzania yanajulikana katika maamuzi yote. Pata habari zaidi na ujiunge na KAMPENI YA CCR YA 50% ILI KUWALINDA WATOTO:

info@50campaign.org
www.50campaign.org

DO YOU KNOW A CHILD WHOSE RIGHTS ARE BEING ABUSED ? CONTACT US.